TANGAZO LA SERIKALI Na. 880 la tarehe. 25/10/2024

SHERIA YA TAFSIRI YA SHERIA,
(SURA YA 1)

# AMRI

(*Imetolewa chini ya kifungu cha 26(3))*

AMRI YA KUREKEBISHA MAKOSA YA KIUCHAPAJI KATIKA KANUNI ZA UWINDAJI WA KITALII ZA MWAKA 2024

Jina na kuanza kutumika
TS. Na. 780 la 2024

**1.** Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurekebisha Makosa ya Kiuchapaji Katika Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2024 na itachukuliwa kuwa imeanza kutumika tarehe 30 Agosti 2023.

Marekebisho ya makosa ya kiuchapaji

**2**. Makosa ya kiuchapaji yaliyomo katika sehemu ya masharti Kanuni za Uwindaji wa Kitalii za Mwaka 2024 yanarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika masharti wezeshi kwa kufuta maneno “kanuni ya” yanayoonekana kati ya maneno “chini ya” na “121(a) na (f)” na badala yake kuweka maneno “kifungu cha”; na

(b) katika kanuni ya 1 kwa kufuta maneno “Utalii wa Uwindaji” yanayoonekana kati ya maneno “Kanuni za” na “za Mwaka 2024 na badala yake kuweka maneno “Uwindaji wa Kitalii”.

Dodoma,
………………., 2024

ONORIUS J. NJOLE,
*Mwandishi Mkuu wa Sheria*